MTAALA WA UMILISI

KUTATHMINI HATUA YA MWANAFUNZI

GREDI 4 - MWAKA 2023

SHUGHULI ZA KISWAHILI

STEP FLYER 002

4

Muda:Saa 1 Dak 40

SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI

1. Umepewa kijikaratasi hiki cha maswali na karatasi ya majibu. Kijikaratasi hiki kina maswali 30.
2. Katika karatasi ya majibu hakikisha umeandika:-
   (i) Jina lako *(ii) Jina la shule yako* *(iii). Nambari ya Knec*

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 1-5.

Kabla ya kwanza kufua nguo hakikisha una besheni, sabuni maji safi na mahali pa kwanika. Hakikisha kuwa kuna jua au upepo. Usipange kufua nguo wakati mvua inanyesha. Tenga nguo zinazotoa rangi na zile ambazo hazitoi rangi. Tenga pia nguo chafu sana kutoka kwa zile ambazo si chafu sana usifue soksi na hanchifu pamoja. Soksi huwa na uchafu mwingi.

Mimina maji ya kutosha kwenye besheni. Tia sabuni kipimo kinachotosha, kama ni sabuni ya unga. Koroga maji hadi povu liwe jingi weka nguo zako kwenye besheni ukitanguliza zile nyeupe. Sugua nguo zako taratibu ukiangazia zaidi sehemu zenye uchafu. Sugua mpaka ziwe safi.

1. Ni kipi hakihitaji kati ya hivi unapoanza kufua nguo?
A. Sabuni
B. Maji safi
C. Beseni
D. Jokofu

2. Ni wakati gani mwafaka wa kufua nguo? Wakati
A. wa mvua
B. wa jua au upepo
C. kuna mawingu
D. kuna jua

3. Ni vazi lipi halifai kufulia pamoja na mengine?
A. Soksi
B. Rinda
C. Hanchifu
D. Kapturà

4. Kwa nini unafaa kukoroga maji baada ya kuongeza sabuni ya unga?
A. Ili povu liwe jingi
B. Ili kutoa nguo chafu
C. Ili maji yawe safi
D. Ili kupasha maji joto

5. Ni sehemu ipi katika nguo inayofaa kusuguliwa zaidi unapofua nguo?
A. Sehemu nyeupe
B. Sehemu iliyo chafu
C. Sehemu yenye doa
D. Sehemu iliyo na rangi